

# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL2

## KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS

### SEHEMU A (Alama 20 )

#### USHAIRI : LAZIMA

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.  
Parapanda tunapiga, kuwaita insani,  
  
Mtindo tukauiga, wa usafi wa rohoni,  
  
Mlungula kiusaga, tutakuwa furahani,  
  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate  
  
Kadhongo ina uvundo, afisini na nyumbani,  
  
Inauponda upendo, nchi yawa masikini,  
  
Hizi njia kandokando, zatuletea huzuni,  
  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.  
  
Hongo kweli ni shetani, huibi unaletewa,  
  
Tamaa kiwa rohoni, kiletewa wachukuwa,  
  
Hujali miko kazini, hela fukoni watiwa,  
  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.  
  
Naye boshi kikudai, kitu kidogo aombe,  
  
Jua huyo hakufai, mashaka yasikukumbe,  
  
Akisema 'leta chai', mpe chai kwa kikombe,  
  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.  
  
Nchi bila mlungula, wanakenya tutapaa,  
  
Mlungula kutokula, wakulima watang'aa,  
  
Tusiwapore kwa hila, tuwalipe kwa wasaa,  
  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.  
  
Barabara tajengeka, za orofa kama Thika,  
  
Usafiri tanyooka, uchumi taimarika,  
  
Wajenzi kiwajibika, wakenya tachangamka,  
  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.  
  
Elimuni tutang'aa, wa kupasi watapasi,

Wapewe kwanza wasaa, wajaze bora nafasi,  
Wasifanyiwe hadaa, kutwaa zao nafasi,  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.  
Kaditama twakuaga, mwananchi mzalendo,  
Sasa ni bega kwa bega, mlungula weka kando,  
Maadili kiyaiga, hatutapata vishindo,  
Maganja mejaa vundo, tuyaoshe yatakate.

- (a) Tambua bahari mbili za shairi hili kwa kuzingatia vina na mishororo. (alama 2)
- (b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili kwa misingi ya neno 'parapanda'. (alama 3)
- (c) Mbinu ya udamisi imetumiwaje katika utungo huu? (alama 2)
- (d) Mtunzi wa shairi ana mtazamo hasi kuhusu suala rejelewa. Fafanua. (alama 2)
- (e) Huku ukitoka mifano, eleza dhima mbili za uhuru wa ushairi katika utungo huu. (alama 2)
- (f) Andika beti za tano na sita kwa lugha tutumbi. (alama 6)
- (g) Ubeti wa pili una toni gani? (alama 1)
- (h) Mshororo, 'Hongo kweli ni shetani, huibi unaletewa' una maana gani? (alama 2)

## **SEHEMU B (Alama 20 )**

### **RIWAYA K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea. Jibu swali la 2 au la 3.**

- 2. 'Kama nakuelewa ndugu yangu, unataka kuleta mapinduzi.'
  - a) Weka dondoo hili katika muktadha wake, (alama 4)
  - b) Jadili mbinu na athari za mapinduzi katika riwaya ya kidagaa kimemwozea. (alama 16)
- 3. Riwaya Kidagaa Kimemwozea imesheheni masuala ibuka katika jamii ya kisasa. Jadili.

## **SEHEMU C (Alama 20 )**

### **TAMTHILIA Timothy Arege:Mstahiki Meya Jibu swali la 4 au la 5.**

- 4. 'Mzee alifahamu kuwa sisi ndio wenye uwezo na tunamfaa.'
  - a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
  - b) Onyesha vile dhana ya kufaa na kujifaa inavyojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 16)
- 5. a) Onyesha juhudi za ukombozi katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 10)  
b) 'Meya anasema baraza la cheneo ni thabiti na halifananishwi na ujirani' Onyesha kinyume katika kauli hii. (alama 10)

## **SEHEMU D (Alama 20 )**

**; HADITHI FUPI K. W. Walibora na S. A. Mohamed (Wah.): Damu Nyeusi na Hadithi Nynyingine. Kikaza (Robert Oduor) Jibu swali la 6 au la 7. 6**

6. "Uniulie nini na ndoa yetu na wewe inamhusu pia yeye?"

(a) Eleza muktadha wa nukuu hii. (alama 4)

(b) Hatima ya mazungumzo ya dondoo hili ni nini? (alama 4)

(c) Jadili changamoto zozote tano ambazo zinawakabili wanajamii katika asasi ya ndoa kwa mujibu wa hadithi Mwana wa Darubini. (alama 12)

7. Ukirejelea hadithi zozote tano katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi nyingine, onyeshavile suala la dhuluma dhidi ya wanawake linavyojitokeza katika hadithi hizo.

## **SEHEMU E (Alama 20 )**

### **FASIHI SIMULIZI: Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

9.

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,

Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,

Anakufanya upite ukinitemea mate,

Chakula kuninyima,wajukuu kinikataza ushirika'

Miungu nawaone chozi langu, wasikie kilio changu,

Mizimu nawaone uchungu wangu, Radhi zao wasiwahi kukupa,

Laana wakumiminie, Uje kulizwa mara mia na wanao,

Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,

Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,

Wakazawanao wasikuunguze katika utu uzima wako!

#### **MASWALI**

a) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

b) Tambua nafsineni katika utungo huu. (alama 1)

c) Eleza sifa tano za kipera hiki. (alama 10)

d) Ni nini umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 4)

e) Eleza umuhimu wa kukusanya data za fasihi simulizi. (alama 4)